# UNATAKA KUSHIRIKI KATIKA MRADI WA UTAFITI

## *«Mwongozo wa wazazi kwa familia zilizo na asili ya wakimbizi»*?

Hii ni ulizo kwako wewe kama mzazi. Tunatafuta wazazi ambao wako tayari kujiunga na mradi wetu wa utafiti ili kuchunguza ufanisi wa mipango ya mwongozo wa wazazi ya familia za wakimbizi hapa nchini Norway.
Hati ama karatasi hii inakuambia kila kitu unachohitaji kujua kuhusu malengo ya mradi na ushiriki unahusisha nini.

## MALENGO

Madhumini na lengo la utafiti huu ni kutathmini na kwangalia ufanisi wa ndani wa mpango wa mwongozo wa wazazi Miaka ya Ajabu “De Utrolige Årene (DUÅ)” na Programu ya Kimataifa ya Maendeleo ya Watoto «International Child Development Programme (ICDP)» inayolenga jamii za wakimbizi. Utafiti huu utachunguza pia matokeo ya mfumo wa maoni yatakayo tumiwa na huduma zinazofanya kazi na wakimbizi.

Katika mpango wa utangulizi wa masomo ya wakimbizi (Introduksjonsprogrammet), kutatolewa mpango wa Mwongozo wa wazazi miongoni ya mambo mengine. Utafiti huu utatusaidia kuongeza elimu na ujuzi zaidi kuhusu ufani wa mipango ya mwongozo wa wazazi “DUÅ” na “ICDP” kwa wazazi na watoto wa wakimbizi. Tungependa kupata majibu na maoni yako kama mhusika wa mpango huu. Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza kama mipango ya mwongozo wa wazazi inasaidia mwingiliano mzuri na kwahivyo kupunguza matokeo ya malenzi mabovu kwa watoto. Tutazungumza na wazazi, watoto, na viongozi wa vikundi vya mwongozo wa wazazi ili kujifunza zaidi kuhusu uzoefu wao na tafakari zao.

## NANI ANAONGOZA MRADI HUU WA UTAFITI?

Kituo cha ujuzi wa afya ya akili za watoto na vijana (RKBU Nord) ya chuo kikuu cha masomo Arctic Norway (UiT) kina wajibu wa kuendesha mradi huu. Mradi huu ni ushirikiano kati ya kituo cha ujuzi wa afya ya akili za watoto na vijana (RKBU Nord), na pia RKBU Midt-Norge katika chuo kikuu cha masomo ya sayansi cha Trondheim NTNU (Norges Teknisk-Naturvitenskapelige Universitet), RKBU West katika kituo cha utafiti cha Norway (NORCE), kituo cha mkoa cha afya ya akili ya mtoto na vijana (Regionssenter for barn og unges psykiske helse /RBUP) mashariki na kusini ya nchi, na kituo cha umahiri cha usaidizi na kinga ya wazazi (SKM). Zaidi ya hayo, pia tunashirikiana na idara ya IMDI (Integrasjons- og mangfoldighetsdirektoratet) na ma offisi yenye kuhusika na huduma za wakimbizi (flyktningetjenestene), na idara ya watoto na familia (Bufdir), eneo la kusini mashariki, wote wana shiriki katika mradi huu.

## SABABU LA KUSHIRIKI?

Umeulizwa kushiriki katika utafiti huu sababu mkoa wako umekubali kushiriki katika mradi huu wa utafiti. Familia zote za wakimbizi zinazoishi kwenye mkoa huu kwa miaka kenda iliyopita wana alikwa kushiriki. Kwa jumla tunahitaji ushiriki wa ma familia takriban 352 yanayo watoto wa umri wa miaka 6 kwenda 12.

## USHIRIKI WAKO UNA MAANISHA NINI?

Tunawauliza tu wanaoshiriki kwa mipango ya mwongozo wa wazazi “DUÅ” na “ICDP” kushiriki katika utafiti huu. Tutagawana vikundi viwili vya wazazi watakaoshiriki kwa njia wa ya bahati nasibu. Kwenye kikundi kimoja cha mwongozo wa wazazi, tutajaribu mfumo wa maoni (MFS) ili tuone jinsi wazazi wanavyoishi na mwongonzo wanaopewa. Wanaoshiriki watahitaji kujibu maswali fulani kila wiki. Majibu hayo yatawekwa tayari kwa viongozi wa vikundi vya mwongozo wa wazazi.

Kwa kushiriki katika utafiti huu kuna maanisha uta jaza orodha ya maswali ya utafiti huu. Tunahitaji ridha idhini (ruhusa) yako ili tuweze kuwasiliana na mwalimu wa mtoto wako tuweze kupata majibu ya kumhusu mtoto wako na tabia zake shuleni.

Katika utafiti huu, tutachagua vikundi tofauti vya wazazi, watoto na viongozi wa vikundi ili tuwahoji. Ndio sababu tunaomba idhini yako kwa kuhudhuria mahojiano haya. Tunahitaji pia ruhusa kutoka kwako ili mtoto wako aweze kuhudhuria mahojiano ya maswali. Baada ya kupata idhini yako, tutaomba mtoto wako idhini yake pia kabla yake mtoto kuhudhuria mahojiano haya.

Wakati huu wa mikutano hii ya mpango wa mwongozo wa wazazi «DUÅ», tunachukua filamu (video) ya mikutano yote. Katika utafiti huu, watafiti, viongozi wa vikundi na viongozi wengine wataangalia filamu hizo. Ni kwa sababu hiyo tunakuomba wewe mshiriki utukubalie kupiga filamu ya mikutano ya vikundi. Unaweza kusoma zaidi juu ya maelezo ya idhini ya ruhsa hapa chini.

## MWONGOZO WA WAZAZI

Mpango wa mwongozo wa wazazi Miaka ya Ajabu «De Utrolige Årene (DUÅ)» na Programu ya Kimataifa ya Maendeleo ya Watoto «International Child Development Programme (ICDP)» ni mafunzo yanayo saidia wazazi kua na mwingiliano mzuri na watoto wao. Mafunzo haya huimarisha uwezo wa wazazi kuweka mipaka mizuri kwa watoto wao na kuimarisha uhusiano mwema kwenye malezi ya mtoto.

Mpango wa mwongozo wa wazazi Miaka ya Ajabu «De Utrolige Årene (DUÅ)» hutumia zana na vyombo mbalimbali kusaidia mzazi azingatie zaidi tabia nzuri za mtoto na pia kuzingatia kidogo tabia mbaya. Kuzingatia tabia nzuri, hujenga mahusiano mazuri na huweka msingi bora wa uhusiano mzuri kwa wale tunaowapenda (kwa mfano, mtoto wako). Mafunzo hayo hufanyika katika makundi ya wazazi yakiongozwa na kiongozi wa kikundi. Wazazi wanazungumzia juu ya hali na changamoto ambazo wazazi wanakabili katika maisha yao ya kila siku.

Mambo yanayo jadiliwa na vikundi yanahusu wakati wa mtoto kucheza na hata pia wakati wa pekee, kumsifu mtoto, kutatua matatizo pamoja na umakini. Ni mafunzo ya vitendo ambapo viongozi wa kikundi na wazazi huunganisha nguvu kujadili na kutafakari malengo ambayo wazazi huweka kwa watoto wao na familia zao. Mafunzo hutumia filamu za video lakini kuanza kwanza na mazoezi ya vitendo kama a mahali pa kuanzia masomo na majadiliano na kutafakari. Viongozi wa kikundi wanazungumza Kinorwe, lakini mkalimani atakuwepo kusaidia kutafsiri kama inahitajika. Vikundi mara nyingi huwa na wazazi ambao hawazungumzi Kinorwe bado, kwa hivyo kuna mara nyingi kadhaa wakalimani waliopo. Wakalimani wote hutia saini Makubaliano ya Kutofichua ili kulinda faragha ya siri yako.

Programu ya Kimataifa ya Maendeleo ya Watoto «International Child Development Programme (ICDP)» ni mpango wa kukuza afya na kinga ambaye inakusaidia kuimarisha utunzaji na malezi ya watoto na vijana. ICDP ni programu ilioanzishwa hapa Norway na inalenga wazazi na wanao lea watoto. Programu hii inasaidia na kuwezesha mzazi katika ulezi wa watoto wao, na za kujenga daraja kati ya maadili ya mbinu asili za ulezi wawatoto na maadili ya katika jamii ya ki norway. ICDP inasisitiza jinsi wazazi na walezi wanavyowachukulia watoto, na inajaribu kukuza uhusiano chanya na mtazamo chanya kwa watoto. Ratiba hii ina mada nane ya mwingiliano mzuri pamoja na vifaa vya kuinua ufahamu kuhusu maana ya mwingiliano mazuri kati ya watoto na wazazi. Mada manane hayo inazingatiya hisia, maoni na maendeleo ya utambuzi, na udhibiti wa kihisia. Mafunzo ya ICDP inaweza kutolewa kwa lugha ya washiriki bila msaada wa mkalimani ikiwa mumoja wa wasimamizi huongea lugha moja na washiriki , ama kwa njia ya mtafsiri. Kila wiki mutapewa zoezi ya nyumbani inayo husiana na mada munayo tumika nayo mu kigundi lenyu. Mtu anaye chunga watoto anapatikana wakati wa kipindi, na chakula kinatolewa kwa ajili yako na mtoto wako.

## MFUMO WA MAONI

Kama sehemu mpango wa utafiti, tutachunguza kama mfumo wa maoni MFS inaweza kusaidia viongozi wa vikundi kurekebisha mwongozo wa wazazi ulingane na mahitaji ya wazazi. Maswali ni kuhusu uzoefu wako na mwongozo wa wazazi.

Katika vikundi ambavyo vitajaribu mfumo wa maoni, wazazi watajibu maswali kumi na mbili katika programu ya APP moja kila wiki. Programu ya APP kwa simu inaweza kuchukuliwa kwa aina zote za simu mahiri. Majibu yanatumwa kwa viongozi

wa kikundi ambao wanapata maelezo ya jumla ya mtu binafsi na maendeleo ya kikundi na kutambua mahitaji ya msaada. Majibu yako pia yatatumika kwa madhumuni ya utafiti.

### UCHUNGUZI KUPITIA FOMU ZA MASWALI

Ukichagua kushiriki katika mradi huu, basi utajaza dodoso mara nne wakati wa masomo ya utafiti: kabla ya mwongozo wa wazazi kuanza, wakati unaendelea, mara tu baada ya kumalizika na tena mwaka mmoja baada ya kushiriki katika mwongozo. Maswali ni kuhusu wewe, unatoka wapi, hali yako ya kazi, afya yako ya afya ya akili, jinsi unavyomlea mtoto wako, jinsi unavyoshughulikia tabia mbaya kutoka kwa mtoto wako, na tabia ya mtoto wako. Inaweza kuwa nyeti kwako kujibu baadhi ya maswali haya.

Hojaji inatumwa kielektroniki kwa kukutumia kiungo kwa SMS au barua pepe. Inachukua takriban dakika 60 kukamilisha fomu. Kama shukrani kwa muda unaotumia, tunalipa NOK 200 kwa njia ya kadi ya zawadi unapomaliza ya tatu (baada ya vikundi kukamilika) na ya nne (mwaka mmoja baada ya vikundi kukamilika) ukusanyaji wa data. (NB: Mkusanyiko wa data unaweza kuhusisha hojaji kadhaa kujibu.)

Pia tutamwomba mwalimu wa mtoto kutoa taarifa fulani kuhusu mtoto wako katika dodoso. Maswali ni kuhusu mtazamo wa tabia na ujuzi wa mtoto wako.

### MAHOJIANO

Ili kupata maarifa kuhusu uzoefu na tafakari za wazazi na watoto, tutawahoji wazazi 40 na watoto 40. Wazazi wataulizwa kuhusu uzoefu wa kushiriki katika mwongozo wa wazazi na kuhusu kuwa mkimbizi na mgeni nchini Norway. Watoto wataulizwa kuhusu uzoefu wao wa kuja katika nchi mpya, mnachofanya kama familia na jinsi mnavyomlea mtoto. Unaweza kuuliza kuona maswali tutakayomuuliza mtoto wako kabla ya mahojiano. Mahojiano hayo yanafanywa kwa msaada wa mkalimani ili atafsiri, na katika mazingira ambayo yanachukuliwa kuwa salama na mazuri kwa mtoto na na hata pia mtu mzima. Mahojiano nawe na mtoto wako yatarekodiwa kwa sauti.

Wazazi au watu wazima wengine kama vile walimu wanaweza kuwepo wakati mtoto anapohojiwa ikiwa inatakikana.

### VIDEODATA

Tunataka upataji wa rekodi hizi za video za mwongozo wa wazazi ili kuangalia mienendo ya vikundi. Pia tutaangalia umuhimu wa kutumia mkalimani atafsiri katika mwongozo wa wazazi.

## NI HIARI YAKO KUSHIRIKI

Ingawaje mpango wa mwongozo wa wazazi ni sehemu ya lazima katika mpango wa utangulizi wa masomo ya wakimbizi (Introdukjsonsprogrammet), ni hiari kwako kushiriki katika mradi wa utafiti (utafiti kupitia dodoso, mahojiano na/au video). Ukichagua kushiriki katika mradi wa utafiti, unaweza kuondoa idhini yako wakati wowote, bila kutoa sababu yoyote.

Ukijiondoa kwenye mradi, unaweza kudai kwamba maelezo yaliyokusanywa yafutwe, isipokuwa maelezo tayari yamejumuishwa katika uchanganuzi au kutumika katika machapisho ya kisayansi.

Hakuna matokeo mabaya kwako, hali yako hapa nchini au hali yako ya kifedha ikiwa hutaki kushiriki katika utafiti huu au ungependa kushiriki na baadaye ukachagua kujiondoa.

Ukijiondoa kwenye utafiti kabla ya kozi ya uzazi kuisha, haitakuwa na athari yoyote kwa ushiriki wako zaidi katika kozi hiyo. **Ili kuondoa idhini chako kutoka kwa utafiti, muone msimamizi wa mradi, Joshua Patras**, pirm@uit.no (maelezo hapa chini)

## FARAGHA YAKO - JINSI TUNAVYOHIFADHI NA KUTUMIA MAELEZO YAKO

Tutatumia tu habari kukuhusu wewe kwa madhumuni ambayo tumeelezea katika taarifa hii. Tunashughulikia habari kwa usiri na kwa mujibu wa kanuni za faragha za siri. Katika kituo cha ujuzi wa afya ya akili za watoto na vijana (RKBU Nord), kikundi cha mradi na timu ya usaidizi wa utafiti pekee ndio wataweza kufikia data yako. Kwa kuongeza, ni watafiti tu,

wafanyakazi wa mradi na timu zao za usaidizi katika taasisi zinazoshirikiana ndizo zinazoweza kufikia maelezo yako ya kibinafsi.

Ili kuhakikisha kuwa data yako imehifadhiwa kwa njia salama, tunatumia Nettskjema kama kichakataji data na TSD - Huduma za Data Nyeti katika Chuo Kikuu cha Oslo kama nafasi ya kuhifadhi kwa dodoso na mahojiano. Jina lako na maelezo ya mwasiliani hubadilishwa na msimbo ambao umehifadhiwa kwenye orodha iliyotengwa ya majina ambayo huwekwa mahali tofauti na data nyingine katika fomu iliyosimbwa kwa njia fiche katika TSD.

Mahojiano yote yamenakiliwa na Totaltekst As.

Kila mtu anaechakata maelezo yako ana jukumu la usiri na haitawezekana kukutambua wewe au mtoto wako kwa jina katika matokeo ya utafiti.

## NINI KINATOKEA KWA MAELEZO YAKO TUNAPOMALIZA MRADI WA UTAFITI HUU?

Mradi umepangwa kukamilika tarehe 31.12.2030. Orodha ya viungo, maelezo ya mawasiliano na maelezo mengine ambayo yanaweza kutambulika moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja yatafutwa miaka mitano baada ya utafiti kukamilika, 31.12.2035. Hii ina maana kwamba haitawezekana tena kutambua taarifa hiyo ni ya nani kwa jina na majibu na taarifa zinazohusiana na wewe na familia yako hazitaweza kuunganishwa nawe.

## HAKI ZAKO NA ZA MTOTO WAKO

Ilimradi wako na mtoto unaweza kutambuliwa katika nyezo za data, mna haki ya:

- Upatikanaji na ujionee taarifa zako za kibinafsi zisajiliwa kukuhusu wewe na mtoto wako (pia taarifa kukuhusi zinazotolewa na waalimu)
- Kusahihisha taarifa za kibinafsi kukuhusu wewe na mtoto wako
- Kuomba taarifa zako na mtoto wako za kibinafsi zifutwe
- Kupata nakala ya maelezo yako ya kibinafsi (ubebaji wa data), na
- Kutuma malalamiko kwa ombudsman ya faragha za siri au Mamlaka ya Ulinzi ya ukusanyaji wa Data nchini Norway kuhusu uchakataji wa data yako yakibinafsi na ya mtoto.

## HASWA NI KITU GANI KINATUPATIA HAKI YA KUCHAKATA TAARIFA ZA KIBINAFSI KUKUHUSU WEWE NA MTOTO WAKO?

Tunachakata maelezo kukuhusu wewe na mtoto kulingana na idhini yako.
Kamati ya Mkoa ya Maadili ya Utafiti wa Tiba na Afya (REK) imetathmini mradi huo, na imetoa kibali cha awali 6852 (22/10/2019)
Kwa niaba ya chuo kikuu cha masomo UiT - Chuo Kikuu cha Arctic cha Norway, NSD - Kituo cha Norway cha Data ya Utafiti AS kimetathmini kuwa uchakataji wa data ya kibinafsi katika mradi huu ni kwa mujibu wa kanuni za faragha za siri.

## JE, UNAWEZA KUPATA HABARI ZAIDI WAPI?

Ukiwa na maswali yeyote kuhusu mradi huu, ama ungependelea kutumia haki zako tafadhali muone kando uwasiliane na msimamizi wa mradi:

- Regionalt kunnskapssenter for barn og unge Nord (RKBU Nord) kwa Joshua Patras, kwa barua pepe: pirm@uit.no ama simu: 776 46 265,
- NSD – Norsk senter for forskningsdata AS, kwa barua pepe: personverntjenester@nsd.no ama simu: 55 58 21 17.
- Ikiwa unahitaji kuzungumza na wataalamu kuhusu hali yako, unaweza kuwasiliana na huduma ya afya ya eneo lako, daktari/mganga au mshauri wa huduma za wakimbizi.

Kwa salamu za fadhili,
Meneja wa mradi, Joshua Patras

# FOMU YA IDHINI

Nimepokea, nimesoma na nikaelewa taarifa juu ya mradi wa "Mwongozo wa wazazi kwa familia zilizo na asili ya wakimbizi" na nimepewa nafasi ya kuuliza maswali.

**Nakubali kushiriki kwa mradi wa PIRM unaojumuisha:**

- kujibu fomu za maswali
- kuchukuliwa filamu nikishiriki kwenye mpango wa mwongozo wa wazazi
- kwamba taarifa zangu za kibinafsi na taarifa za kibinafsi za mtoto wangu zinachakatwa na kuhifadhiwa hadi mwisho wa mradi huu
- kwamba majibu yangu yatahifadhiwa katika hali isiyotambulika baada ya mwisho wa mradi

| | |
|---|---|
| | • Ndiyo, nakubali |
| | • Hapana, sikubali |

Ninakubali kwamba mwalimu wa mtoto wangu atatoa taarifa kuhusu mtoto wangu kwa mradi huu (ikiwa mtoto anahuzuria shule)

| | |
|---|---|
| | • Ndiyo, nakubali |
| | • Hapana, sikubali |

Nakubali kushiriki kwenye mahojiano ikiwa hii itakuwa muhimu

| | |
|---|---|
| | • Ndiyo, nakubali |
| | • Hapana, sikubali |

Nakubali kuwa mtoto wangu ahojiwe kama hii itakuwa muhimu

| | |
|---|---|
| | • Ndiyo, nakubali |
| | • Hapana, sikubali |

| Mnaishi katika manispaa gani/ wilaya gani ya mji? |
|---|
| |
| Jina lako nani? (jina la kwanza na jina la mwisho) |
| |
| Tarehe na saini |
| |

**TAFADHALI ENDELEA KWENYE UKURASA UNAOFUATA**

| Jinsia yako ni gani? | |
|---|---|
| | Kike |
| | Kiume |
| Ulizaliwa mwaka gani? | |
| | |
| Namba yako ya simu ya rununu ni gani? | |
| | |

**Chagua mtoto wako mkubwa aliye kati ya umri wa miaka 6 hadi 12.** Isipokuwa wewe, kuna mtu mwingine anayeishi nchini Norway ambaye ana jukumu la mzazi kwa mtoto wako? (kama vile mzazi mwingine)

☐ Ndiyo ☐ Hapana

| Jina la mtu huyu ni gani? (jina la kwanza na jina la la mwisho) | |
|---|---|
| | |
| Ni jinsia gani ya mtu huyu? | |
| | Kike |
| | Kiume |
| Mtu huyu alizaliwa mwaka gani? | |
| | |
| Je, mtu huyu pia atashiriki katika mpango wa mwongozo wa wazazi? Kama ndiyo, tungependa kumwalika mtu huyu kujiunga na utafiti wa PIRM. | |
| | Ndiyo, mtu huyu atashiriki katika mpango wa mwongozo wa wazazi |
| | Hapana, mtu huyu hatashiriki katika mpango wa mwongozo wa wazazi |

Tunaomba sasa uongeze taarifa yako ya mawasiliano, ya mtoto wako na ikiwezekana ya mzazi mwingine/mlezi kwa kunakili na kubandika kiungo hiki kwenye kivinjari chako: **https://nettskjema.no/a/pirm-kontaktinfo-swahili**

Baada ya kujaza taarifa ya mawasiliano kuhusu familia yako kwenye kinvinjari, tafadhali tuma FOMU YA IDHINI (ukurasa wa 5 na wa 6) kwa:

***UiT Norges arktiske universitet***
***Postboks 6050 Langnes***
***Helsefak, RKBU NORD, PIRM prosjektet***
***9037 Tromsø***